**Issue no:** 1 | **Vol no:** 5 | **September**2024: 32-39

# Mitindo ya Mawasiliano katika Kipindi cha Patanisho, Redio Jambo Nchini Kenya

**Irvine Songok** [(1)]
**Lina Akaka** [(2)]
**Rose Mavisi** [(3)]

(1.2.3) Catholic University of Eastern Africa, Kenya
Main author email: ivysongok91@gmail.com

**Article History**
Received: 2024-07-02
Accepted: 2024-08-08
Published: 2024-09-19

**Cite this article in APA**
Songok, I., Akaka, L., & Mavisi, R. (2024). Mitindo ya mawasiliano katika kipindi cha Patanisho, Redio Jambo nchini Kenya. *Editon Consortium Journal of Kiswahili*, *5*(1), 32-39. https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v5i1.533

**Ikisiri**

Lengo la makala hii ni kuchanganua mitindo ya mawasiliano inayotumiwa na manahodha wa kipindi cha Patanisho cha Redio Jambo nchini Kenya. Kipindi cha Patanisho cha Redio Jambo ni mojawapo ya vipindi vya redio vinavyoendeleza majukumu yake kama asasi inayowaunganisha wasikilizaji kupitia kwa mijadala inayohusu masuala ya kijamii. Utafiti huu umevutiwa na diskosi za migogoro ya kifamilia zinazoendeshwa na manahodha wa kipindi cha Patanisho, Redio Jambo.Watafiti wa makala hii walipania kuchunguza jinsi manahodha wa kipindi hiki wanavyotumia mitindo ya mawasiliano ili kuvutia umakinifu wa wasikilizaji. Utafiti ulifanywa kwenye mtandao wa Youtube wa idhaa ya Redio Jambo. Muundo wa utafiti ni wa kimaelezo. Kikundi lengwa cha utafiti ni kipindi cha Patanisho, Redio Jambo. Sampuli za utafiti ziliteuliwa kimaksudi. Jumla ya vipindi 60 vya Patanisho vilivyopeperushwa hewani kati ya miezi ya Januari na Aprili 2023 katika Redio Jambo na kurekodiwa kwenye Youtube vilisikilizwa na watafiti na vipindi 10 vikateuliwa kimaksudi kwa misingi ya mitindo ya mawasiliano iliyomo. Mtafiti alikusanya data kwa kusikiliza na kunakili. Vifaa vya ukusanyaji data vilivyotumiwa ni tarakilishi, daftari na kalamu. Data ilichanganuliwa kimaelezo. Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa mitindo tofauti ya mawasiliano hutumiwa na manahodha wa kipindi kujenga mahusiano na kuvuta umakinifu wa wasikilizaji. Watafiti walibaini kuwa mitindo ya mawasiliano inayotumiwa na manahodha wa kipindi hufanikisha malengo ya kipindi chenyewe. Matokeo ya utafiti huu yanatoa changamoto kwa manahodha wa vipindi vya redio kubuni mitindo na mikakati mipya ya mawasiliano itakayowavutia wasikilizaji wa vipindi vyao na kubuni vipindi vinavyoshughulikia changamoto wanazokumbana nazo wanajamii katika maisha.

**Maneno muhimu**: Mitindo, mlaumiwa, mpigasimu, nahodha, redio.

Editon OPEN ACCESS

This article is distributed under the license of a Creative Commons Attribution-Non Commercial-ShareAlike 4.0 International License. It is permitted to be used, reproduced and distributed in line with Editon Consortium Publishing guidelines.

## UTANGULIZI

Mtindo wa mawasilino ni upekee wa jinsi mtu anavyowasiliana na wengine (Liu, 2016). Dhana ya mtindo huhusisha viashiria vya lugha. Upekee wa mtindo wa mawasiliano ya mzungumzaji huelekeza jinsi msikilizaji hupokea na kufasiri ujumbe kupitia lugha. Makala hii ilishughulikia mitindo inayotumiwa na manahodha wa kipindi cha Patanisho cha Redio Jambo nchini Kenya. Redio ni mojawapo ya vyombo vya habari vya zamani sana. Kulingana na Bowen (2010), wakenya wengi wanatumia redio kupata habari na matangazo mbalimbali. Redio za hivi karibuni zina programu anuwai zinazowaruhusu wasikilizaji kupiga simu na sauti zao kusikilizwa wanaposhirikishwa katika mijadala. Kwa kufanya hivi, redio ya leo imeathiri mabadiliko ya kijamii.

Redio Jambo ni mojawapo ya redio nchini Kenya zinazoendesha vipindi vinavyowapa wasikilizaji fursa ya kufichua changamoto wanazopitia katika maisha yao ya kila siku. Baadhi ya vipindi kama hivyo ni Barua ya Milele cha Milele FM, Mahakama 47 cha Redio 47 na Msamaha cha Redio Maisha na kadhalika. Wasikilizaji wa kipindi cha Patanisho kama vile vingine vilivyotajwa awali, hupewa nafasi ya kupiga simu na kufafanua mizozo inayotokea kati ya wanafamilia na suluhu ya mizozo hiyo kupatikana baada ya mazungumzo na manahodha. Diskosi zinazohusu masuala ya kijamii hususan mahusiano ya kifamilia huendelezwa katika kipindi hiki. Mitindo inayotumiwa na manahodha wa kipindi hiki kushawishi wasikilizaji wanaopiga simu kufungua mioyo na kueleza matatizo katika mahusiano yao ndiyo haswa iliyovutia watafiti kuichanganua. Dhana ya uchanganuzi wa diskosi ni pana; hurejelea miktadha mbalimbali, lugha inayotumika, mikakati inayotumiwa kuvuta umakini, mitindo katika mawasiliano, uenezaji wa propaganda, uimarishaji wa kaida za jamii. Tafiti nyingi zilizotangulia zilichunguza diskosi katika masuala ya vita na siasa. Utafiti huu ulichunguza diskosi zilizomo katika kipindi cha Patanisho cha Redio Jambo. Diskosi katika kipindi hiki zinahusu masuala ya kijamii hususan changamoto za mahusiano ya kifamilia. Hivyo basi, watafiti walichunguza namna manahodha wa kipindi hiki wanavyotumia mitindo mbalimbali ya mawasiliano kuwahusisha wasikilizaji wanaopiga simu katika mazungumzo kuhusu masuala mbalimbali ya kijamii. Uchunguzi ulionyesha kuwa mitindo hii huwasaidia manahodha kujenga mahusiano na wasikilizaji na kuvuta umakinifu wao. Makala hii ilijadili mitindo inayotumiwa na manahodha wa kipindi cha Patanisho, Redio Jambo na miktadha ambamo imetumika.

## MAPITIO YA MAANDISHI

### Mitindo ya Mawasiliano katika Diskosi za Vipindi vya Redio

Onsarigo na wenzake (2020) walifanya utafiti kuhusu uchanganuzi wa mitindo ya uwasilishaji katika vipindi teule vya vituo vya redio na athari zake kwa lugha ya Kiswahili nchini kenya. Sampuli za utafiti zilikuwa leksimu za sheng zilizopeperushwa hewani na Redio Citizen, Redio Maisha na Redio KBC. Utafiti wao uliongozwa na nadharia ya uchanganuzi wa sajili ya Halliday (1978). Matokeo ya utafiti wao yalibaini kuwa matumizi ya sheng na ubadilishaji msimbo ni mtindo wa uwasilishaji wa vipindi katika vituo vya redio. Hivyo mtindo huo una athari kubwa kwa lugha ya Kiswahili kwa sababu hutumiwa zaidi kama mtindo wa mawasiliano ili kuvutia usikilizaji katika vituo vya redio hizo.

Altrov na wenzake (2023) walitafiti mitindo ya semi za matangazo ya redio miongoni mwa wasikilizaji walio na lugha tofauti za kwanza nchini Estonia. Lengo la utafiti wao lilikuwa kutambua iwapo wasikilizaji katika jamii ambazo kuna jamii kubwa ya watu walipendelea kusikiliza matangazo ya redio kwa kutumia lugha ya kitaifa sawia na wasikilizaji wasio wa jamii kubwa. Vikundi vyote viwili vilisikiliza matangazo ya redio yaliyowasilishwa katika lugha ya Kiestonia na watu mbalimbali. Matokeo ya utafiti wao yalionyesha kuwa vikundi vyote viwili vilipendelea mtindo wa utulivu. Walihitimisha kwamba ni vyema kutambua mitindo ya kuwasilisha matangazo katika jamii ambazo watu wana lugha tofauti za kwanza kwa sababu iliafikia malengo ya utangazaji bora.

Habwe (1999) alifanya utafiti uliohusu uchanganuzi wa mazungumzo ya hotuba nane za kisiasa nchini Kenya. Mtafiti alishughulikia kipengele cha maana katika mazungumzo hayo, ukweli, dhana ya upole na ucheshi. Mtafiti alionyesha kuwa ucheshi katika

hotuba za kisiasa ulikuwa mtindo wa mawasiliano uliotumika sana ili kupunguza hali tata katika mikutano ya kisiasa. Utafiti wake ulibaini kuwa katika baadhi ya matukio, ucheshi ulitumiwa kama jukwaa la kuwasilisha mambo mazito yaliyosemwa ili kufurahisha hadhira bila athari kubwa au maudhi yoyote.

Uchanganuzi wa mazungumzo uliofanywa na Kiai (1996) ulilenga uchambuzi wa rejista za mijadala ya programu zilizowaelimisha wakulima. Mtafiti alifanya uchambuzi wa kileksia na wa kimtindo wa matini za redio zilizoandikwa na jinsi lugha ilivyotumiwa katika mazungumzo ya redio. Mtafiti alitumia nadharia ya tendouneni. Sampuli ya utafiti ilikuwa programu hamsini ambapo programu thelathini na saba zilitumika kupata data ya utafiti huo. Uchanganuzi wa kileksika wa utafiti wa Kiai (1996) ulibaini kuwa vipindi vya redio vilihusisha leksmimu zilizorahisishwa kileksika kupitia mitindo ya mawasiliano kama vile uigaji na kuchanganya msimbo. Mtafiti alionyesha kuwa mitindo hii ya kileksia iliwezesha lugha za asili kutumika kama njia ya kufunzia katika programu iliyotafitiwa.

Inya na wenzake (2018) walitafiti kuhusu ucheshi katika mazungumzo ya habari za redio mbili nchini Nigeria. Utafiti wao ulilenga kuonyesha hatua ambazo ucheshi ulitokea katika habari hizo. Data ya utafiti wao ilijumuisha rekodi za sauti ya masaa kumi kutoka kwa vituo viwili vya redio nchini Nigeria. Matokeo ya utafiti yalibainisha aina nne za ucheshi zilizotumiwa kuwavutia wasikilizaji wa habari za redio hizo.

## MBINU ZA UTAFITI

Muundo wa uchanganuzi huu ni wa kimaelezo. Utafiti huu ulifanyika maktabani na pia katika mtandao wa YouTube kati ya miezi ya Januari 2023 na Aprili 2023. Mtandao wa YouTube uliteuliwa kimaksudi kwa kuwa vipindi vya Patanisho hupakuliwa pale. Hili lilirahisisha shughuli ya kuvinakili kwa kuwa mtandao wa Youtube una vifaa vya kurejesha nyuzi nyuma na kupunguza kasi ya mazungumzo. Watafiti walikusanya data kutoka kipindi cha Patanisho cha Redio Jambo kwa kuvisikiliza na kuvinakili vipindi 60 vya Patanisho. Hatimaye, vilipitiwa kwa makini na vipindi 10 vikateuliwa kimaksudi kwa misingi ya aina ya mitindo ya mawasiliano iliyomo ili kutafitiwa. na nadharia ya uchanganuzi hakiki wa matini kwa mujibu wa Fairclough (1995) ikatumiwa kuchanganua data kimaelezo. Uchanganuzi huu hujikita katika matini iliyoandikwa au kusemwa. Fairclough (1995) aliibua kielelezo chenye safu tatu ambacho kinafafanua namna matini inavyochanganuliwa. Kwa mujibu wa Fairclough & Wodak (1997), uchanganuzi wa kina wa matini huhusisha kutambua vipengele vya lugha, kuvifasiri na kufafanua vile vinavyotokea kwa kuangazia miktadha ya kijamii. Mhimili wa 'diskosi huhusisha ufasiri na ufafanuzi' ulitumiwa kuchanganua mitindo ya mawasiliano katika kipindi cha Patanisho cha Redio Jambo. Watafiti waliongozwa na taratibu za mhimili huu zilizohusisha kutambua jinsi lugha ilivyojitokeza katika viwango vya sarufi na sinaksia. Pili, walifasiri jinsi mazungumzo hayo yalivyotolewa na kusambazwa na jinsi yalivyofasiriwa na msikilizaji wa kipindi kisha wakafafanua mitindo ya mawasiliano baina ya manahodha na wasikilizaji ilivyojitokeza.

## MATOKEO YA UTAFITI

Waandishi wa makala hii walibaini kuwa manahodha wa kipindi cha Patanisho cha Redio Jambo hutumia mitindo tofauti kuendeleza mazungumzo katika kipindi hicho. Manahodha wa kipindi cha Patanisho hutumia mitindo kama ukatizwaji, ucheshi, ulazima wa kutoa majibu, sajili ya kimamlaka na mengineyo. Manahodha wa kipindi hiki hutumia mtindo wa sajili ya kimamlaka kuwashawishi wazungumzaji kuzungumza ili ujumbe unaohitajika ujitokeze. Kwa mfano, katika hali nyingi, nahodha wa kipindi humtaka mpigasimu kuwa na uchache wa maneno, usahihi na uwazi anapojieleza. Aidha, ucheshi hutumiwa kushughulikia masuala ya kutisha kama uchawi. Nahodha huwakatiza wazungumzaji ili kuhakikisha kuwa hawachukui muda mwingi katika masuala yasiyohusiana na mada au anapokubaliana nao. Mitindo mbalimbali wanayotumia manahodha wa kipindi ili kuvutia idadi ya wasikilizaji wengi itajadiliwa katika sehemu zifuatazo.

### Ucheshi

Mtindo wa mawasiliano wa nahodha wa kipindi pia ulibainika kuwa wa kiucheshi na kukifanya kipindi kiwe cha kuburudisha na kuvutia usikilizwaji. Dziegielewski na wenzake (2003) wanaeleza kuwa

DRAFT

ucheshi hufanya zaidi ya kuwafanya watu wacheke. Ucheshi humfanya mtu kuungana na hadhira, kuinua hali, kueneza mvutano, na vile vile kulazimisha wengine kuvutiwa kwa mtazamo wa mtu. Zaidi ya hayo, ucheshi ukitumiwa vizuri unaweza kumsaidia mtu kuupinga ujumbe wake. Ucheshi haumaanishi kuwa mada inayojadiliwa haina uzito. Badala yake, ni chombo chenye nguvu ambacho huongeza uhusiano baina ya watu wanaowasiliana.

Ucheshi pia una jukumu muhimu katika kuhakikisha kwamba masuala ya kutisha yanashughulikiwa kwa njia isiyo ya kutisha. Ikiwa baadhi ya masuala hayakushughulikiwa kwa ucheshi, inaweza kuwa vigumu kuyatatua. Kwa mfano, suala la uchawi lililotajwa katika mfano ufuatao linaweza kuwa gumu la kujadili lakini mjadala huo ukiambatanishwa na vicheko unarahisisha suluhu kupatikana. Kwa hivyo, inaweza kuwa vigumu kushughulikia masuala kama haya isipokuwa yakishughulikiwa kwa vicheko. Katika mfano huo, mpigasimu anasema “Niliona mganga akakuja akafinya kuku, akapeperusha damu kisha nikajikuta sio mimi tena." Kisha anaendelea kuelezea sifa za mganga yule “Huyo mganga alikuwa mubaba hivi, mrefu, hakuwa amevalia mguuni kitu chochote.” Maelezo ya mganga huyo yanajitokeza kama ya kuchekesha, jambo ambalo linawachekesha wasikilizaji wengine. Maelezo hayo ya kuchekesha yanawaburudisha na kuwaacha na wakitaka kusikiliza visa vingine kama hivyo.

**Ukatizwaji**

Mojawapo ya mikakati ya kipragmatiki inayozingatiwa katika uchanganuzi wa mwingiliano kati ya mwasilishaji na msikilizaji ni ukatizwaji. Kukatizwa kwa mazungumzo hutokea pale ambapo nahodha anakatiza kauli za mzungumzaji. Nahodha anaweza kukatiza kauli ili kubainisha maelezo anayotafuta. Kwa hivyo, ukatizwaji kauli hufanyika nahodha anapotaka ufafanuzi dhahiri wa suala. Ukatizwaji huonyesha kwamba habari anazotoa mzungumzaji sizo zinazohitajika. Hivyo basi nahodha huchukua fursa hiyo kutoa mwelekeo kwa mzungumzaji ili kuhakikisha kuwa hawachukui muda mwingi katika masuala yasiyohusiana na mada inayojadiliwa.

Ingawa watu wengi wanaona kukatizwa kama jambo baya katika mazungumzo, matokeo yalionyesha kuwa unaweza kutumika kujenga ushirika badala yake. Kulingana na vipindi vilivyochanganuliwa, kuna madhumuni mawili makuu ya zamu. Mojawapo ni kukamilisha zamu ya kila mmoja. Kulingana na matokeo na majadiliano, ni dhahiri kwamba kuwepo kwa udakizo, ama kukamilishana usemi ili kukata zamu ya mzungumzaji mwingine, huakisi mwingiliano wa ushirikiano. Orcutt na Mennella (1995) walitoa maoni kwamba ni jambo la kawaida kwa washiriki katika mazungumzo ya kawaida kuchangizana kauli wakati huo huo kama aina ya kitendo cha ushirika.

Ukatizwaji unapotokea, unaweza kufasiriwa kwa njia nyingi kulingana na muktadha. Waandishi wa makala haya walibaini kuwa wingi wa ukatizwaji katika kipindi cha Patanisho hufichua maarifa yaliyoshirikiwa pamoja na mtazamo sawa wa washiriki. Inafahamika kuwa wazungumzaji wanaoshiriki maarifa sawa na pia mtazamo sawa wanaweza kukamilisha au kupunguza zamu za kuzungumza za wenzao. Kwa mfano, wasemaji ambao wameshiriki maarifa wanaweza kukamilisha zamu ya kila mmoja kwa urahisi au kukatiza matamshi ya wenzao ili kutoa jibu. Mazungumzo katika dondoo lifuatalo yanadhihirisha hali hiyo:

> **Mlaumiwa**: Mimi nishapata mwanamume mwingine tayari niko na mimba. Sasa…
> **Nahodha**: Ah! Tayari una mimba?

Katika dondoo hilo, ukatizwaji unajitokeza katika alama za dukuduku zinazokuja baada ya neno sasa na kauli ya nahodha iliyofuatia ukatizwaji huo. Nahodha alikatiza kauli hiyo kwa nia ya kutaka kufafanuliwa zaidi alilolisema mlaumiwa Ufafanuzi huo ungemsaidia kushughulikia suala lililopo kwa uwazi zaidi.

Wakati mwingine ukatizwaji unaweza kutumika nahodha anapotaka kumwelekeza mpigasimu kutoa taarifa zinazohitajika. Kwingineko katika dondoo lifuatalo, ukatizwaji hautumiki kufafanua bali kumwelekeza mpigasimu kutoa taarifa zinazohitajika. Mpigasimu ameulizwa swali lakini kwa vile swali limeulizwa kwa njia ambayo itamfanya mpigasimu kufichua habari ambazo pengine hakutaka kufichua, ili kufichua habari ambayo labda hakutaka kuzifichua, anajaribu



DRAFT

kukwepa swali kwa kubadilisha mada. Hata hivyo, nahodha anamkatiza na kumuongoza kuelekea kujibu swali aliloulizwa kama inavyojitokeza katika mfano huu:

> **Nahodha**: Bwana Steve, kati ya hao wanawake wote umeenda nao nje kunaye ambaye yuko na mtoto wako?
> **Mpigasimu**: Bwana Gidi….
> **Nahodha**: Ah! Ah! Nijibu.

Kukatizwa kunaweza pia kuonyesha makubaliano na usaidizi (Smith, 2015). Hili linapotokea, pande mbili zinazohusika zinaonyesha kwamba zinakubaliana juu ya jambo moja na kukatizwa huko kunaweza kuchukuliwa tu kuwa njia ya kuonyesha makubaliano kati ya pande mbili zinazohusika.

> **Nahodha**: Wakati mzee aligawa shamba alipata shamba lake ama hakuwa anataka Job apate?
> **Mlaumiwa**: Job alipewa shamba lake…
> **Nahodha**: Kwa hivyo alipewa shamba lake pale nyumbani na tayari yuko na shamba?

Nahodha anapokatiza kauli ya mlaumiwa, anakusudia kukubaliana naye kwamba kaka yake tayari ana shamba ambalo anapaswa kutumia kwani ni sehemu ya urithi wake. Ni vyema kutambua kwamba taarifa za awali kuhusu urithi zilishirikiwa na nahodha na kwa hivyo, kukatiza kwake kunachukuliwa kuwa makubaliano na msaada kwa msikilizaji kuhusu suala hilo.

**Utoaji Majibu kwa Kulazimishwa**

Kulazimisha ni mbinu inayotumika katika nyanja za kisheria na uandishi wa habari ili kuwafanya watu watoe taarifa zinazohitajika. Ikiwa habari inayohitajika haiwezi kupatikana kupitia njia za kawaida, watu hulazimishwa kutoa habari kama njia inayopendekezwa ili kuhakikisha kuwa habari imepatikana. Maswali yanaweza kuwa ya kuhitaji jibu la ndio au hapana au ya kutoa ufafanuzi wa kina. Hata hivyo, maswali ya aina hii hayahitaji taarifa zozote kwa vile tayari huwa zimekwishatolewa na jibu hutumika tu kwa shughuli za kulisaili zaidi. Kwa mfano, Nahodha anapouliza “Kwa nini wewe ulimnyang’anya shamba ndugu yako?” inaashiria kwamba nahodha ana habari ya kutosha kuhusu hilo jambo na kile ambacho angetaka ni jibu kutoka kwa anayeulizwa.

Blommaert na Bulcaen (2000) wanakubali kwamba maswali yanatumika kama njia ya kupata habari na vile vile kutoa udhibiti. Licha ya hayo, maswali yanayotolewa kama tangazo huwa yanatumiwa kutoa taarifa wakati huohuo yakihitaji. Katika mfano ufuatao, nahodha anamshurutisha mpigasimu kumpa habari bila kumficha lolote:

> **Nahodha:** Kwa nini ulimdhurumu bibi yako?
> **Mpigasimu**: Ni shetani tu lakini nimeamua kubadilika
> **Nahodha**: Haujanijibu swali langu…Ni kweli kwamba ulimtesa bibi yako kwa kumletea wanawake wengine?
> **Mpigasimu**: Ni kweli. Lakini...

Umbo au asili ya swali huwaathiri umbo na maudhui ya jibu litakalotolewa. Isitoshe kumbukumbu za msikilizaji katika mazungumzo ya kipindi cha redio inaweza kuathiriwa na tabia ya nahodha au mitindo yake ya mawasiliano. Hili ni muhimu katika kipindi cha Patanisho ambapo upande mmoja huja kwa nia moja tu ya kutatua matatizo ya wapigasimu au mahitaji yao kushughulikiwa. Kwa hivyo, kwa manahodha wengi wa redio, maswali ni njia ya kumdhibiti msikilizaji ili kuhakikisha kuwa malengo ya kipindi yanafikiwa.

Cameron (2001) anahoji kuwa ushawishi unaweza kupatikana kwa kujumuisha taarifa iliyokusudiwa katika swali na baadaye kupanga swali kwa njia ambayo inalifanya liwe gumu kukanusha. Uteuzi wa aina ya maswali hutegemea uhusiano wa nguvu kati ya watu wawili wenye nguvu zaidi wanaotarajia maswali yao kujibiwa na majibu kulingana na maswali (Gibbons, 2003). Kimsingi maswali ambayo hayana ushurutishwaji wakati wa kujibiwa ni yale yasiyohitaji ufafanuzi ilhali yale ya ushurutishwaji wa kutoa jibu ni yale hutoa tangazo kama inavyojitokea katika mazungumzo yafuatayo:

> **Nahodha**: Na hii hasira kuna vile unaweza icontrol… unajua hiyo ni hasira sana ndugu. Yangu?
> **Mpigasimu**: Unajua shida ni nini Gidi…
> **Nahodha**: Siku hizi watu wanafanya kitu inaitwa anger management
> **Nahodha**: Unapaswa uende upewe ushauri ndio hiyo hasira yako uweze kuicontrol.
> **Mpigasimu**: Yes
> **Nahodha**: Kwa hivyo itabidi wewe ujichunge ndio uweze control hiyo hasira yako.

Katika huo mfano, nahodha huchukua muda mwingi huku akimpa mpigasimu muda mchache wa

kujieleza. Nahodha anamkashifu na kumkemea mpigasimu kwa kumpiga mkewe na anaonyesha kutoridhika na viwango vya hasira yake. Kwa hivyo, nahodha amechukua jukumu kubwa la kutawala mjadala. Kimsingi, nahodha anachukua nafasi ya mamlaka zaidi. Ili kufanikiha mchakato huo wa upatanisho, wahusika wote lazima wahusishwe kikamilifu katika majadiliano kulingana na kanuni za nadharia ya mawasiliano. Licha ya uwajibikaji huu wa pamoja, wawasilianaji huwa na nguvu tofauti katika mawasiliano. Kwa mfano, katika kipindi cha Patanisho, nahodha ndiye anayebeba mamlaka ya juu zaidi na kuelekeza mwelekeo ambao uamuzi unapaswa kuchukua. Kama mshiriki mkuu, nahodha anaamua ni nani azungumze wakati gani na kwa muda gani.

**Burudani**

Rodero (2020) anaeleza ya kwamba manahodha wa redio huburudisha wasikilizaji na watazamaji wao. Walakini, manahodha wa kipindi cha Patanisho hawaburudishi tu bali hushauri na kutatua migogoro vilevile. Kipindi cha Patanisho ni tofauti. Kinashauri, kinatatua migogoro na kuburudisha kwa wakati mmoja. Kimsingi, hukejeli maovu ndani ya jamii hasa katika masuala ya ndoa na familia na kutumia maridhiano na vichekesho kama nyenzo za kuyashughulikia. Burudani, ingawa si dhamira kuu ya kipindi, huja ili kufifisha uzito wa suala linaloshughulikiwa, na kumfanya msikilizaji aweze kujihisi huru zaidi kujieleza na kuwatia moyo washiriki kujihusisha kwa njia ya kirafiki. Kwa mfano, katika dondoo lifuatalo, mazungumzo yanaendelezwa ifuatavyo:

> **Mpigasimu**: ...mimi nilitoka nyumbani miaka kama ishirini iliyopita
> **Nahodha**: Sasa ulikuwa unakaa wapi na ukifanya nini?
> **Mpigasimu**: Nilikuwa nakaa Eldoret. Nilikuwa mkora
> **Nahodha**: Ooh, kwa hivyo ulikuwa mkora kazi yako ilikuwa kuwapiga ngeta huko?

Wakati ambapo nahodha anasisitiza kwamba mpigasimu alikuwa mkora na alikuwa akiwaibia watu inaashiria kicheko kwa sababu anapoyasema haya maneno ndipo anamsisimua mpigasimu. Ili burudani ipatikane, haiba ya mtangazaji ina jukumu kubwa na hujitokeza kupitia kwa sauti anayotumia, aina ya maswali anayouliza na pia njia ya mwingiliano wao na msikilizaji. Ni lazima pia ifahamike kwamba manahodha katika kipindi cha Patanisho si wahoji tu bali ni watu ambao huwa sehemu ya hadithi na kuathiri msikilizaji kwa kujihusisha na vicheko vyao vya kuambukiza haswa juu ya masuala yanayochekesha. Licha ya hayo, wanajaribu kutoa nafasi nyingi kwa wapigasimu iwezekanavyo ili kuhakikisha kwamba wana muda zaidi wa kuzungumza na kuwasilisha masuala yao. Kwa mfano, katika dondoo lifuatalo, mazungumzo haya yanaendelezwa ifuatavyo:

> **Mpigasimu**: Alileta mganga nyumbani, nilijirealize after 4 days kuwa niliharibika kichwa.
> **Nahodha**: Huyo mganga alikuwa anakaa aje?
> **Mpigasimu**: Alikuwa mrefu hivi mbaba na hakuwa na viatu…

Katika mfano huu, nahodha wa kipindi anamwelekeza mpigasimu kuelezea taswira ya yule mganga na maelezo ambayo mpigasimu anayatoa yanaibua kicheko si haba. Kwa kusisitiza na kuendeleza kicheko, nahodha anayarudia maneno yayo hayo hali ambayo inafanya msikilizaji acheke zaidi.

**Mtagusano wa Wasikilizaji**

Mtagusano wa mzungumzaji na msikilizaji ni maeneo muhimu ya uchunguzi wa uchanganuzi wa mazungumzo. Ukweli ni kwamba msikilizaji anapotambua na kuelewa maana ya mazungumzo, yeye hushiriki katika mazungumzo hayo. Hivyo yeye huamua kukubaliana au kutokubaliana, kuyatumia na kujiandaa ili kuyatumia miongoni mwa mambo mengine (Chang, 2004). Katika muktadha wa redio, nahodha ana jukumu la kumchochea msikilizaji kuendelea kusikiliza ambako huendeleza mawasiliano yanayofaa. Manahodha haswa ni wawakilishi wa mashirika ya utangazaji na huwa kama viungo kati ya shirika na wasikilizaji. Njia moja ambayo nahodha wa kipindi cha Patanisho hutumia ili kuboresha mtagusano baina ya wasikilizaji na wazungumzaji na kuwahimiza kuendelea kuzungumza ni kutumia maneno kama vile “mmmmh, ndiyo, eeh na endelea” miongoni mwa mengine.

Kwa mujibu wa Cotteril (2004) tungo kama vile ‘uh-uh’ na ‘mm-hmm’ hutumika katika mazungumzo kuashiria kukubaliana, kuridhika na vilevile

DRAFT

kuhimiza mtu kuendelea kuzungumza. Inafahamika pia kwamba matumizi ya ‘mm-hmm’ yanaweza kuwa ishara kwamba mhusika hafurahishwi na wazo linalopendekezwa. Zaidi ya hayo, yanaweza kuonyesha kuwa wamepumzika sana na wanaweza kukosa nguvu ya kusikika kwa shauku zaidi. Kwa hivyo, maneno kama vile ‘mm-hmm,’ uh-uh na mengineyo yanaweza kutumika kuonyesha kutosheka au raha, kutokuwa na uhakika au kutafakari, au makubaliano au kibali. Ikumbukwe kwamba yote hayo humhimiza msemaji kuendelea kusema. Kwa mfano pale yanapofichua kutokuwa na uhakika, mzungumzaji anahimizwa kuendelea kuzungumza ili kufafanua kauli alizotoa, kwa mfano:

**Nahodha**: Kwa hivyo ulipatikana?
**Mpigasimu**: Ndio nilipatikana
**Nahodha**: Eeh
**Mpigasimu**: Lakini nikamueleza hakuna kitu nilikuwa nimefanya. Ndio ilikuwa imeanza.
**Nahodha**: Ndio ilikuwa imeanzaanza ehh?
**Mpiga simu**: Eeeh. Ndio ilikuwa imeanza.
**Nahodha**: Mm-hmm
**Mpigasimu**: Alikuwa ameniamini sana sasa vile aliona hivyo akakasirika sana
**Nahodha**: Mm-hmm
**Mpigasimu**: Sasa hiyo ikaleta shida akaenda kwao
**Nahodha**: Mm-hmm
**Mpigasimu**: Vile nilirudi hakuwa na hasira yoyote
**Nahodha**: Mm-hmm

Katika dondoo hilo, nahodha anatumia sana maneno kama vile mm-hmm ambayo ni muhimu katika kumhimiza mpigasimu kuendelea kuzungumza. Matumizi ya maneno ‘mmh’ na ‘eeh’ humfanya mpigasimu aridhike kwamba kuna mtu anayemsikiliza. Kwa njia hii, huhimizwa kuendelea kuzungumza. Katika isimu wanazuoni wanaona matumizi ya maneno hayo kama utoaji nafasi kwa mpiga simu ili ajieleze bila kukatizwa. Kadri nahodha anavyoendelea kutumia maneno hayo ndivyo mpigasimu anavyopata motisha ya kuendelea kuzungumza na kufanya mazungumzo yatiririke.

## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

**Hitimisho**: Kutokana na matokeo ya utafiti huu ya kipindi cha Patanisho, ilibainika kuwa mitindo ya mawasiliano ilihusisha mambo kama vile ucheshi, ukatizwaji, utoaji majibu kwa kulazimishwa, mtagusano wa wasikilizaji na burudani. Mara nyingi, nahodha hujitokeza kama mpole na mtulivu. Hutumia sauti ya chini na kumwalika mpigasimu asimulie kisa chake. Aidha, wanatumia ucheshi mwingi wanapowatuliza wanaozozana kutokana na makali ya maneno yao. Manahodha huonyesha mamlaka yao wanapowalazimisha washiriki kufafanua zaidi. Hivyo, humsaidia mpigasimu kusimulia kisa chake na kupata jawabu analohitaji.

**Mapendekezo:** Watafiti wanapendekeza vipindi vingine vya redio vitafitiwe kwa mtazamo huu ili kuchunguza vipiengele vingine vya lugha. Zaidi ya hayo, utafiti zaidi wa vipindi vya mazungumzo baina ya manahodha wa vipindi vya redio na wasikilizaji unapendekezwa. Hapa, nadharia ya uchanganuzi hakiki wa mazungumzo inaweza kupanuliwa ili kujumuisha vipengele vingine kama vile sauti, muziki na ukimya ndani ya vipindi vya redio.

## MAREJELEO


Altrov, R., Pajupuu, H., Pajupuu, J., & Kiisla, A. (2023). Radio Advertisement Speech Style Preferences among Listeners with Different First Languages within One Country. *Frontiers in Communication*, *8*, 1176423.

Blommaert, J., & Bulcaen, C. (2000). Critical Discourse Analysis. *Annual Review of Anthropology*, 29, 447-466. http://www.jstor.org/stable/223428

Bowen, H. (2010). *Information at the Grassroots: Analyzing the Media Use and Communication Habits of Kenyans to Support Effective Development*. InterMedia`s Audience Research Initiative. London and Washington: InterMedia.

Cameron, D. (2001). *Working with Spoken Discourse*. SAGE Publications.

Chang, Y. (2004). Courtroom Questioning as A Culturally Situated Persuasive Genre of Talk. *Discourse and Society*, *15*(6), 705-722. DOI 10.1177/0957926504046501.




DRAFT

Cotteril, J. (2004). Collocation, Connotation, and Courtroom Semantics: Lawyers' Control of Witness Testimony through Lexical Negotiation. *Applied Linguistics*, *25*(4), 513-537.

Dziegielewski, S. F., Jacinto, G. A., Laudadio, A., & Legg-Rodriguez, L. (2003). Humor: An Essential Communication Tool in Therapy. *International Journal of Mental Health, 32*(3), 74-90. http://www.jstor.org/stable/41345062

Fairclough, N. (1995b). *Critical Discourse Analysis*. Longman.

Fairclough, N., & Wodak, R. (1997). *Critical Discourse Analysis*. in T. Van Dijk (Eds). Pp 258-284, Discourse as Social Interaction. Sage.

Gibbons (2003). *Forensic Linguistics: An Introduction to Language in the Justice System.* Blackwell.

Habwe, J. H. (1999). *Discourse Analysis of Swahili Political Speeches*. Doctoral Dissertation: University of Nairobi.

Inya, B. T., & Inya, O. (2018). Conversational Humor in a Nigerian Radio News Programme: A Case Study of Lati Inu aka Biodun/ Kayode. *The European Journal of Humor Research*, *6*(4).

Kiai, A. W. (1996). *A Discourse Analysis of Educational Radio Programmes to Farmers: Adaptations in Register*. Doctoral dissertation.

Liu, M. (2016). *Verbal Communication Styles and Culture*. In Oxford Research Encyclopedia of Communication.

Onsarigo, H. M. (2020). *Mitindo ya Uwasilishaji wa Programu za Redio na Athari Zake katika Lugha ya Kiswahili Nchini Kenya.* Tasnifu ya shahada ya uzamili (haijachapishwa) Chuo Kikuu cha J.O.O.U.S.T.

Orcutt, J. D., & Mennella, D. L. (1995). Gender and Perceptions of Interruption as Intrusive Talk: An Experimental Analysis and Reply to Criticism. *Symbolic Interaction*, *18*(1), 59–72. https://doi.org/10.1525/si.1995.18.1.59

Rodero, E. (2020). Radio: The Medium that Best Copes in crisis. Listening Habits, Consumption, and Perception of Radio Listeners during the Lockdown by the Covid-19. *El Profesional de* UNIVERSITAS AIRLANGGA

Smith, D. L. (2015). Interrupted Speech in Luke-Acts. *Journal of Biblical Literature*, *134*(1), 177–191. https://doi.org/10.15699/jbl.1341.2015.2834